

Taarifa za Uchaguzi Maalum wa Wadi 3 utakaofanyika Tarehe 17 Agosti, 2021

Kura ya Mapema

- Wapiga kura wote, waliosajiliwa katika wadi 3 watatumiwa karatasi za kupigia kura kufikia tarehe 2 Julai.
- Iwapo hautapokea karatasi yako ya kupiga kura kufikia tarehe 12 Julai, tafadhali wasiliana na ofisi ya Katibu/Mhazini kupitia (802) 865-7000 (chaguzi 1) au elections@burlingtonvt.gov
- Fuata maagizo yote kwa makini unapojaza karatasi yako ya kura ya utoro. Hakikisha UMETIA SAHIHI kwenye bahasha na UIFUNGIE karatasi yako ya kura ndani mwake, la sivyo kura yako itakuwa batili.
- Rejeshwa karatasi ya kura uliyotia alama:
 - City Hall Jumatatu hadi Ijumaa, baina ya saa mbili asubuhi hadi saa sita unusu mchana na baina ya saa saba unusu mchana hadi saa kumi unusu jioni ****TAFDHALI ZINGATIA***** kwamba City Hall itakuwa imefungwa mnamo Jumatatu, Tarehe 16 Agosti.
 - Kwenye Sanduku la Kurejeshwa Karatasi za Kura lililopo:
 - City Hall – Upande wa Main Street wa jengo hilo mkabala na Flynn Theater
 - Fire Station #2 – 132 North Avenue, nyuma ya jengo
 - Kwenye kituo cha kupigia kura cha Wadi 3, Sustainability Academy/Lawrence Barnes Elementary School, 123 North St., Siku ya Uchaguzi baina ya saa moja asubuhi na saa moja usiku

Kupiga kura Siku ya Uchaguzi

- Maeneo ya kupigia kura yatakuwa wazi baina ya saa moja asubuhi na saa moja usiku Siku ya Kupiga Kura
- Njoo na karatasi ya kupiga kura ambayo ulitumiwa. Iwapo hukupokea karatasi ya kupiga kura au iwapo utasahau kubeba karatasi ya kupiga kura uliyotumiwa, bado utaweza kupiga kura, lakini utaombwa kujaza na kutia sahihi hati ya kiapo.

Tarehe Muhimu

Julai 2 – Karatasi za Kura kutumwa kwa wapiga kura wote waliosajiliwa

Agosti 13, saa kumi unusu jioni – makataa ya kurejeshwa karatasi yako ya kura pale City Hall

Agosti 16, saa saba mchana – makataa ya kujisajili kupiga kura kabla ya Siku ya Uchaguzi

Agosti 16, saa kumi unusu jioni – makataa ya kurejeshwa karatasi yako ya kura uliyotia alama kwenye sanduku la kurejeshwa karatasi za kura

Agosti 17 – Siku ya Uchaguzi. Vituo vitafunguliwa saa moja asubuhi hadi saa moja usiku